

Kuangua vifaranga mwenyewe

Kuangua mayai ni biashara nzuri kwa wafugaji. Hata hivyo, biashara hii ni hatari sana na kwa hivyo ni lazima mazingatio sahihi yatekelezwe ili kupata mafanikio.

Mayai yasiyorutubishwa hayaanguki na hivyo ni lazima mazingatio yafuatwe ili kuhakikisha kuwa mayai yote yatakayoanguliwa yana rutubishwa ili kuepuka hasara. Mayai kutoka kwa kundi hili hilo la kuku huhakikisha maumbile mazuri ya kuku. Pia mayai ambayo hayafai kuanguliwa yanaweza kutumika kama chakula cha nyumbani.

Mambo ya kuzingatia wakati wa kuangua

Hakikisha unapata mayai kutoka vyanzo vyta uhakika ili kuepuka kununua mayai duni. Baada ya kusafirisha mayai, yaweke mahali penye ubaridi kabla ya kuangushwa.

Kusanya mayai kila wakati katika majira ya masika kwa vile ndio wakati mzuri wa uzazi, uhifadhi wa yai na ukuaji wa vifaranga.

Weka jogoo kati ya majike ili kupata mayai yenye rutuba.

Chambua mayai kulingana na sifa bora, na hifadhi mayai mazuri kwa kiatimizi ili kudumisha maumbile mazuri ya kuku..

Pia weka mayai mahali pasafi na uyasafishe bila kuyasugua kwani kusugua kunaharibu ganda la yai.

Hakikisha unaweka mayai kwenye trei huku sehemu kubwa ya yai ikielekea juu ili kuzuia kupasuka.

Mwishowe, kwa uhifadhi mrefu, inua trei upande mmoja kila siku ili kiini cha yayi kisishikamane na kuta za ganda, na hifadhi mayai kwenye mahali baridi pasipopenyeza jua moja kwa moja ili kuzuia ukuaji wa viini vyta ugonjwa.

Mambo ya kuzingatia wakati wa kuangua yai

Kwanza, ganda la yai linapaswa kuwa safi bila madoa, na pia yai lisiwe dogo sana au kubwa sana kwani mayai madogo hutoa kifaranga dhaifu na mayai makubwa huangua vifaranga wenye kasoro.

Pia ganda la yai lisiwe na ufa, lisiwe na mikunjo na vile vile mayai yasiwe ya duara sana, wala marefu sana. Mayai yasiwe membamba sana ili yaweze kuanguliwa.

Hatimaye, umri wa ndege pia ni muhimu kwa vile ndege wachanga hutoa mayai ambayo huangua vifaranga wagonjwa.